**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.** AB.392/512/01A/38 **Tarehe:** 17/08/2026

Makatibu Wakuu wa Wizara,
Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika ya Umma na Binafsi,
Wakuu wa Idara Zinazojitegemea,
Watendaji Wakuu wa Mamlaka na Wakala za Serikali,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya,
**TANZANIA.**

Ndugu,

**YAH: MWALIKO WA KONGAMANO LA 17 LA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Bodi inafuraha kukutaarifu kuwa itakuwa mwenyeji wa Kongamano la 17 la Mwaka la Ununuzi na Ugavi **tarehe 14 hadi 18 Desemba, 2026 Ngurdoto Mountain Lodge Limited Arusha.** Kongamano hili huwaleta pamoja wadau wote wa shughuli za za ununuzi na ugavi kutoka ndani na nje ya nchi ili kujadili na kubadilishana uzoefu katika masuala ya kitaalamu katika sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuzingatia kaulimbiu isemayo; Mnyororo wa ugavi wa kijani na himilivu na kufikia malengo ya maendeleo endelevu, na utekelezaji wa dira ya taifa 2050. ("***Green and Resilient Supply Chains for Competitive and Sustainable Development Goals and the Realization of National Vision 2050)".***

3. Hivyo, Bodi inakuomba ukiwa kama mwajiri na mdau muhimu wa PSPTB kitaaluma kuwafadhili wataalam wako wa ununuzi na ugavi, wajumbe wa bodi ya zabuni na watumishi wa idara tumizi kutoka fani mbalimbali pamoja na watoa maamuzi wengine wanaohusika katika shughuli za ununuzi na ugavi ili waweze kuhudhuria kongamano hili muhimu. Kongamano hili litawasaidia kubadilishana uzoefu, maarifa na ujuzi mahsusi kwenye mnyororo wa ugavi wa kijani na himilivu.

4. Ni matarajio ya PSPTB kuwa kupitia Kongamano hili washiriki wataweza kuboresha utendaji kazi wao binafsi na taasisi zao ili kuleta tija katika maendeleo ya sekta binafsi na sekta ya umma. Pia, washiriki waliosajiliwa na PSPTB wataidhinishiwa **saa 40** za maendeleo ya kitaaluma (*CPD hrs*) kama hitaji lao la msingi kitaaluma.

5. Kwa wataalamu wote, usajili wa ushiriki ufanyike mtandaoni kupitia akaunti zao za usajili mtandaoni. Washiriki wasio na usajili wa PSPTB, usajili wa ushiriki wao utafanyika mtandaoni kupitia; [https://registration.psptb.go.tz/](https://registration.psptb.go.tz/) kwenye tangazo la kongamano hili. Ada za ushiriki zimefafanuliwa katika jedwali hapa chini:

| Washiriki | Ada ya ushiriki |
|---|---|
| Wataalam waliosajiliwa na PSPTB | TZS. 700,000/= |
| Washiriki wengine | TZS. 850,000/= |
| Wanafunzi wasio na ajira | TZS. 400,000/= |
| Washiriki kutoka nje ya Tanzania | USD 500 |

6. Ada hizi za ushiriki ni kwa ajili ya maandalizi na uwasilishwaji wa mada, nyenzo za kongamano, kifungua kinywa na chakula cha mchana tu. Tafadhali, kumbuka kuwa hakuna washiriki watakaoruhusiwa kuhudhuria mkutano wa kongamano hili bila kukamilisha malipo ya ada za ushiriki zilizotajwa hapo juu. Mwisho wa kulipa ada ya ushiriki ni tarehe 30 Novemba, 2026.

7. Tunakushukuru kwa ushirikiano wako katika kujali taaluma hii adhimu ya ununuzi na ugavi kwa maendeleo ya Taifa.

8. Wasalaam,

Digitally Signed By GODFRED MBANY
Mon Aug 17 18:16:31 EAT 2026

GODFRED MBANYI
**MKURUGENZI MTENDAJI**

*GBM/mim.*

**Kumbuka:**
Vazi rasmi kwa ajili ya ufunguzi ni suti ya rangi ya ***dark blue*.**

*Mkandarasi Place (Ghorofa ya saba), S.L.P. 2663, Dodoma. Simu: +255 22 2865860*
*Nukushi: +255 22 2862138. Tovuti: [http://www.psptb.go.tz](http://www.psptb.go.tz). Barua pepe: [info@psptb.go.tz](mailto:info@psptb.go.tz)*


pspt b
"Committed to Excellence"
17TH PROCUREMENT AND SUPPLY CHAIN PROFESSIONALS ANNUAL CONFERENCE"
THEME
Green and Resilient Supply Chains for a Competitive and Sustainable Development Goals and the Realization of National Vision 2050
DATE
14TH TO 18TH DECEMBER, 2026
VENUE
NGURDOTO-ARUSHA
PARTICIPATION FEES:
• PSPTB Registered Professionals: ............... TZS 700,000.00
• Other Professionals: ............... TZS 850,000.00
• Foreigners: ............... USD 500
• Students: ............... TZS 400,000.00
FOR REGISTRATION
registration.psptb.go.tz
FOR MORE INFORMATION PLEASE CONTACT
+255757311154
PSPTB TV
Bodi Ununuzi
psptbofficial
www.psptb.go.tz